

## KUELEWA IDHINI

### IDHINI NI NINI?

Idhini inaelezwa kama **makubaliano ya hiari** kushiriki tendo la ngono linalojadiliwa. Idhini inapaswa kuwa **na shauku, ya hiari na endelevu**. Idhini au "ndiyo" ambayo inapatikana kwa msukumo, kwa kulazimishwa, kwa nguvu, au kwa ubabe sio ya hiari. Idhini ni kuomba ruhusa. Mtu ambaye ameleta, amepoteza ufahamu au amelala, hawezi kutoa idhini.

JINSI YA KUOMBA IDHINI	NJIA TOFAUTI KUSEMA HAPANA
<ul style="list-style-type: none"> <li>Je, ninaweza kukubusu??</li> <li>Je, utahisi kuwa sawa nikishika mkono wako?</li> <li>Naomba kujaribu mahusiano ya kimapenzi na wewe. Je, mambo haya yanakuvutia? Ni sawa kama hayakuvutii.</li> <li>Je, unasikia vizuri kujaribu _____ na mimi? Usiwe na shurutisho.</li> <li>Nimeona kwamba uko kimya. Je, bado unataka mambo haya?</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Sitaki kufanya ngono.</li> <li>Sihisi vizuri kufanya mambo haya. Tafadhali acha kunigusa.</li> <li>Sitaki kufanya hiyo tena.</li> <li>Asante kwa kunikaribisha nyumbani/kunisindikiza nyumbani. Nataka kuwa wazi kwamba sitaki kufanya ngono sasa hivi.</li> <li>Najua kwamba bado hatujaongea kuhusu hiyo, lakini nataka kuongea kuhusu matarajio juu ya ngono na/au urafiki.</li> <li>Nataka kukujulisha kwamba sipendi kuguswaguswa</li> </ul>
SIKILIZA UJUMBE ZA KUKUBALI ZIFUATAZO:	SIKILIZA UJUMBE ZA KUKATAA ZIFUATAZO:
<ul style="list-style-type: none"> <li>Ndiyo</li> <li>Hisia zangu ni sawa na zako.</li> <li>Mimi nataka wewe u-...</li> <li>Nahisi vizuri kuhusu hiyo.</li> <li>Niko tayari ku....</li> </ul>	<ul style="list-style-type: none"> <li>Acha</li> <li>Hapana</li> <li>Sijui kuhusu...</li> <li>Sina uhakika kuhusu...</li> <li>Sidhani kama niko tayari kwa...</li> </ul>

- |   |   |
|---|---|
| <ul style="list-style-type: none"><li>• Endelea</li></ul> | <ul style="list-style-type: none"><li>• Naogopa</li><li>• Tunaweza kupunguza mwendo?</li><li>• Nadhani nimekunywa sana pombe</li><li>• Nina hofu kuhusu magonjwa ya zinaa na/au VVU</li></ul> |
|---|---|

**Sikiliza ujumbe zisizo za maneno zifuatazo:**

kama yule mwingine amesogeza mwili wake mbali nawe; kama yule mtu "ameganda" au hasogezi mwili wake; au kimya.